

**GRADE 2 END TERM 3 DECEMBER 2021  
KISWAHILI ACTIVITIES**

**1. UFAHAMU (Alama 10)**

**1. Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata:(Alama 5)**

Mimi ninaitwa Salim. Ninaishi na baba na mama yangu. Nina dada na kaka mmoja. Mimi hucheza na binamu yangu. Sisi humtembelea ami mashambani. Mimi hufurahia hadithi za nyanya na babu..

- a) Mimi ninaitwa nani? \_\_\_\_\_ (alama 1)
- b) Ninaishi na nani? \_\_\_\_\_ (alama 2)
- c) Sisi humtembelea nani mashambani? \_\_\_\_\_  
(alama 1)
- d) Ni nani hutupatia hadithi za kufurahisha? \_\_\_\_\_  
(alama 1)

**2. Soma hadithi kisha ujibu maswali yanayofuata (alama 5)**

Siku ya Jumamosi Tito na Tom walienda kuwinda ndege msituni. Huko msituni waliona mnyama akija karibu na wao. Tito na Tom walipiga mayowe. Watu walikuja kuwasaidia. Tito na Tom walipelekwa nyumbani. Wazazi waliwaeleza kuwa msituni kuna wanyama hatari. Tito na Tom waliomba msamaha.

- (a) Tito na Tom walienda msituni siku gani? \_\_\_\_\_  
(alama 1)
- b) Walienda msituni kufanya nini? \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_ (alama 1)
- c) Waliona nini wakiwa katika msitu? \_\_\_\_\_ (alama 1)
- d) Ni nani waliwasaidia? \_\_\_\_\_ (alama 1)
- e) Wazazi wao waliwaeleza nini? \_\_\_\_\_ (alama 1)


2. **SARUFI**

(Alama 15)

1. **Andika majina ya vyombo hivi vya usafiri.**


(Alama 5)

a)



\_\_\_\_\_

b)




\_\_\_\_\_

c)




\_\_\_\_\_

d)



\_\_\_\_\_

e)



\_\_\_\_\_

2. **Unda maneno ukitumia silabi hizi (alama 5)**

a) nga \_\_\_\_\_

b) re \_\_\_\_\_

c) chu \_\_\_\_\_

d) nyu \_\_\_\_\_

e) gha \_\_\_\_\_

3. Jibu maamkizi haya.

(Alama 3)



a) Hujambo? \_\_\_\_\_

b) Shikamoo? \_\_\_\_\_

c) Habari? \_\_\_\_\_

4. Andika hali hizi za anga

(alama 2)



\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

3. KUANDIKA: IMLA

(Alama 10)

Andika sentensi tano utakayosomewa na mwalimu wako

1. \_\_\_\_\_

2. \_\_\_\_\_

3. \_\_\_\_\_

4. \_\_\_\_\_

5. \_\_\_\_\_

## 1. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (Alama 5)

***Sikiliza hadithi nitakayokusomea kisha nitakuuliza maswali.***

Halima na Zainabu walikuwa wanafunzi katika shule ya Mkombozi. Walikuwa katika Gredi ya pili. Mwalimu mkuu Bwana Juma aliwahimiza kusoma kwa bidii. Halima alikuwa mvivu sana. Siku moja alichelewa kuamka. Halima alikataa kwenda shuleni. Siku iliyofuata alipoenda shuleni aliadhibiwa. Halima aliamua kubadilika.

- a) Halima na Zainabu walisomea shule gani?(**alama 1**)
- b) Walikuwa katika gredi gani?(**alama 1**)
- c) Mwalimu mkuu aliitwa nani?(**alama 1**)
- d) Mwalimu mkuu aliwahimiza nini? (**alama 1**)
- e) Ni nani alichelewa kuamka? (**alama 1**)

## 2. KUSOMA KWA SAUTI (alama 10)

***Soma hadithi hii kwa sauti.***

Mimi ninaitwa Petero. Mimi ni mvulana. Nina shida ya macho. Macho yangu hayaoni vizuri. Nina dada wawili. Mmoja anaitwa Nekesa na mwingine anaitwa Nasieko. Nekesa anasoma katika Gredi ya tano. Nasieko yuko katika gredi ya tatu.

Mimi niko katika gredi ya pili. Wazazi wetu wanatupenda sana. Wao hutunulia chakula ili tuwe na afya bora. Wazazi wetu hutupeleka hospitalini tukiwa wagonjwa.